



(Mawasiliano yote yafanyike kupitia
kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali)

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.: AC 334/376/01/383

Tarehe: 08 Oktoba, 2026

YALIYOJITOKEZA

FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI SEPTEMBER, 2026

1. MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

1.1 Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa (FBT) ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Kapu linalotumika kukokotoa FBT lina jumla ya bidhaa 383 ambazo bidhaa 132 ni za Vyakula na Vinywaji Baridi, na bidhaa 251 ni bidhaa zisizo za vyakula. Kwa wigo wa kijiografia, FBT zinakokotolewa kwa kutumia takwimu za bei zinazokusanywa kwenye makao makuu ya mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

1.2 Mizania za Fahirisi na Kizio

Mizania za Fahirisi za Bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa maeneo ya mijini na vijijini. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18 yalitumika kama chanzo kikuu cha takwimu za uandaaji wa mizania za Fahirisi. Kizio cha Bei cha Fahirisi zilizofanyiwa marejeo kimeboreshwa na kuwa wastani wa bei za mwezi Januari hadi Disemba 2020, na kizio cha Fahirisi ni mwaka 2020.

1.3 Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa zinatumia mpangilio wa kimataifa wa matumizi binafsi ujulikanao kama COICOP "Classification of Individual Consumption by Purpose" wa mwaka 2018. Aidha, Fahirisi za Bei zinatolewa kwenye makundi 13 ya mpangilio wa COICOP, 2018 pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu ambayo yanajumuisha: - Fahirisi za msingi (*core index*); Fahirisi ya nishati, mafuta na huduma za maji; Fahirisi isiyo ya msingi (*Noncore index*); Fahirisi ya huduma; Fahirisi ya bidhaa; Fahirisi ya huduma za elimu na bidhaa zinazoambatana nazo na Fahirisi ya bidhaa zote isiyojumuisha bidhaa za vyakula na vinywaji baridi.

1.4 Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi za mwanzo unatumia wastani wa jiomertia "geometric mean of Price Relatives". Kanuni ya Fahirisi ya *Lowe Index Formula* ambayo ni aina ya "Laspeyres Index Formula" hutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

2 MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KWA MWEZI SEPTEMBER, 2026 UMEFIKA ASILIMIA 4.3**Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Septemba, 2026, (2020 = 100)**

Na.	MAKUNDI MAKUU YA FAHIRISI	Mizania (Weight)	Septemba., 2025	Agosti., 2026	Septemba., 2026	Badiliko la mwezi mmoja	Badiliko la miezi 12
1	Vyakula na Vinywaji Baridi	28.2	129.70	135.36	134.70	-0.5	3.9
2	Vinywaji Vikali na Tumbaku	1.9	113.60	114.62	114.86	0.2	1.1
3	Mavazi na Viatu	10.8	115.09	116.89	117.01	0.1	1.7
4	Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo	15.1	118.48	121.08	121.47	0.3	2.5
5	Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi	7.9	116.99	119.39	119.98	0.5	2.6
6	Afya	2.5	109.60	111.14	111.14	0.0	1.4
7	Usafiri	14.1	120.78	136.18	137.66	1.1	14.0
8	Habari na Mawasiliano	5.4	106.31	107.88	107.93	0.0	1.5
9	Burudani, Michezo na Utamaduni	1.6	111.10	111.98	111.70	-0.3	0.5
10	Huduma za Elimu	2.0	111.99	115.55	115.55	0.0	3.2
11	Migahawa na Huduma za Malazi	6.6	117.39	120.79	120.79	0.0	2.9
12	Huduma za Bima na Fedha	2.1	102.34	102.58	102.59	0.0	0.2
13	Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko	2.1	118.30	122.26	122.22	0.0	3.3
JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE		100.0	119.86	124.93	125.07	0.1	4.3
Makundi Mengine Teule							
1	Fahirisi za Msingi (<i>Core Index</i>)	73.9	116.36	120.74	121.18	0.4	4.1
2	Fahirisi Isiyojumuisha Fahirisi za Msingi (<i>Non-Core Index</i>)	26.1	129.81	136.83	136.13	-0.5	4.9
3	Fahirisi za Nishati, Mafuta na Bili za Maji	5.7	131.86	141.85	142.09	0.2	7.8
4	Fahirisi za Huduma	37.2	113.16	119.34	120.05	0.6	6.1
5	Fahirisi za Bidhaa	62.8	123.83	128.24	128.05	-0.2	3.4
6	Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu	4.1	114.40	116.42	116.39	0.0	1.7
7	Bidhaa zote isipokuwa bidhaa za chakula na bidhaa za vinywaji visivyo na kilevi	71.8	116.00	120.84	121.30	0.4	4.6

2.1 Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa Kipimo cha Mwaka

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 linaonesha kuwa, kiwango cha Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2026 kilibaki kuwa asilimia 4.3 sawa na kiwango kilichorekodiwa kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026. Hii ina maana kuwa kiwango cha jumla cha ongezeko la bei za bidhaa na huduma katika mwaka ulioishia Septemba 2026 kilikuwa sawa na kiwango kilichorekodiwa katika mwaka ulioishia Agosti 2026. Fahirisi za Bei zimeongezeka kutoka 119.86 mwezi Septemba, 2025 hadi 125.07 mwezi Septemba, 2026, ikionesha ongezeko la jumla la bei za bidhaa na huduma kati ya Septemba 2025 na Septemba 2026.


2.2 Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2026 umeongezeka hadi asilimia 3.9 kutoka asilimia 3.7 kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei ambao haujumuishi Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Septemba, 2026 umebaki katika asilimia 4.6 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026.

2.3 Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (Core Inflation)

Fahirisi za bei za msingi zinaandaliwa kwa kutojumuisha bidhaa za vyakula zisizochakatwa; nishati na bili za maji. Kutojumuisha bei za bidhaa ambazo zina sifa ya kubadilika mara kwa mara kwenye Fahirisi za bidhaa na huduma zote, hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera. Fahirisi za bei za msingi zinakokotolewa kwa kutumia bei za bidhaa na huduma 297 na mchango wa mizania kwenye Fahirisi zote ni asilimia 73.9. Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (Core inflation) kwa mwezi Septemba, 2026 umebaki katika asilimia 4.1 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti, 2026.

Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Septemba, 2025 hadi Septemba, 2026. (2020 = 100)



Kielelezo Na. 1 kinaonesha kuwa, Fahirisi za Taifa ya Bei zimekuwa na mwelekeo wa kuongezeka kati ya Septemba 2025 na Septemba 2026, ambapo ziliongezeka kutoka 119.86 mwezi Septemba 2025 hadi 125.07 mwezi Septemba 2026. Katika kipindi hicho, Kiwango cha Mfumuko wa Bei wa Jumla kwa mwaka kilibaki katika kiwango cha wastani, kikibadilika kati ya asilimia 3.2 na asilimia 4.3. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa, wakati Fahirisi za Bei ziliongezeka kwa ujumla katika kipindi hicho, Kiwango cha Mfumuko wa Bei kilibadilika ndani ya kiwango kidogo, ambapo kiwango cha juu cha asilimia 4.3 kilirekodiwa mwezi Agosti 2025 na Septemba 2026.

3 FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KATI YA MWEZI AGOSTI 2026 NA SEPTEMBER, 2026

Fahirisi za Bei za Taifa kati ya mwezi Agosti, 2026 na Septemba, 2026 zimeongezeka kutoka 124.93 hadi 125.07. Kuongezeka kwa Fahirisi za Bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: mtama kwa asilimia 0.1; unga wa ngano kwa asilimia 0.3; kuku wa kienyeji kwa asilimia 0.2; nyama ya kuku kwa asilimia 0.1; samaki wabichi kwa asilimia 1.7; maziwa ya ngombe kwa asilimia 0.8; mafuta ya kupikia kwa asilimia 0.3; karanga mbichi kwa asilimia 1.5; viazi vitamu kwa asilimia 3.9; mihogo mibichi kwa asilimia 2.0; maghimbi kwa asilimia 0.5; ndizi mbichi kwa asilimia 3.7; maharage kwa asilimia 0.4; choroko kwa asilimia 1.8; njegere kavu kwa asilimia 3.1; unga wa muhogo kwa asilimia 3.9 na vinywaji baridi jamii ya soda kwa asilimia 1.4. Kwa upande mwingine baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa Fahirisi za Bei ni pamoja na: vinywaji vikali na tumbaku kwa asilimia 0.2; vitambaa vya kushona nguo kwa asilimia 1.2; nguo za wanaume kwa asilimia 0.1; nguo za wanawake kwa asilimia 0.1; viatu vya wanaume kwa asilimia 0.3; viatu vya wanawake kwa asilimia 0.4; viatu vya watoto kwa asilimia 0.1; saruji kwa asilimia 3.9; mabati kwa asilimia 1.1; vigae vya sakafuni kwa asilimia 0.5; gesi kwa matumizi ya kaya kwa asilimia 1.7; nishati ya kuni kwa asilimia 4.6; samani za nyumba kwa asilimia 0.5; nauli za taksi kwa asilimia 1.9 na nauli za pikipiki/bodaboda kwa asilimia 5.8.

Jedwali Namba 3: Ratiba ya Utangazaji Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijaye.

Fahirisi za Bei za Taifa	Tarehe ya Toleo
Oktoba, 2026	09 Novemba, 2026
Novemba, 2026	08 Desemba, 2026
Desemba, 2026	08 Januari, 2027